HOTUBA YA MHE. KAPT. (MST.) GEORGE HURUMA MKUCHIKA (MB) WAZIRI WA NCHI, OFISI YA WAZIRI MKUU, TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA WAKATI WA KUFUNGA MAONYESHO YA MAADHIMISHO YA MIAKA HAMSINI YA UHURU KWA OFISI YA WAZIRI MKUU TAREHE 12 OKTOBA 2011, KATIKA VIWANJA VYA MNAZI MMOJA

Waheshimiwa Mawaziri Wakuu Wastaafu

Waheshimiwa Mawaziri,

Waheshimiwa Naibu Mawaziri;

Mhe. Mkuu wa Mkoa wa Dar es Salaam

Waheshimiwa Wabunge,

Makatibu Wakuu Wastaafu

Mheshimiwa Mstahiki Meya wa Jiji la Dar es Salaam,

Waheshimiwa Mameya wa Manispaa za Kinondoni, Ilala na Temeke,

Waheshimiwa Makatibu Wakuu

Watumishi wa Ofisi ya Waziri Mkuu,

Wageni Waalikwa,

Mabibi na Mabwana,

Awali ya yote, napenda kutumia fursa hii kuwashukuru Wananchi ambao wametembelea maonesho ya Ofisi ya waziri Mkuu kwa wingi tangu siku ya uzinduzi hadi leo hii tunapoyafunga rasmi. Kuja kwenu kwa wingi

kutembelea maonesho haya, kunathibitisha shauku mliyonayo ya kufahamu shughuli zinazotekezezwa na Ofisi ya Waziri Mkuu na pia kupata maelezo ya mafanikio ambayo Serikali imeyapata katika kipindi cha miaka 50 ya Uhuru. Ni mategemeo yangu kwamba maonesho haya yamesaidia kuwapa mwanga wa yale makubwa yaliyofanyika pamoja na changamoto zilizopo mbele yetu ambazo tunaendelea kuzikabili kwa nguvu zote.

Napenda niwashukuru kwa kunialika kufunga maonesho haya. Aidha, niwashukuru Mawaziri Wakuu Wastaafu na viongozi mbalimbali wastaafu waliowahi kuongoza Ofisi ya Waziri Mkuu kwa kukubali kutenga muda wao kutembelea maonesho haya. Wametupa moyo kwamba wako nasi katika jitihada za kusukuma gurudumu la maendeleo ya Taifa kwenda mbele. Aidha, ushiriki wao umewezesha kuitangaza vyema ofisi ya Waziri Mkuu na kuwezesha wananchi kutambua vyema mafanikio mbalimbali tuliyokwisha yapata tangu tujipatie uhuru wetu. Nawashukuru pia waheshimiwa Wabunge ambao walikuwa nasi siku ya ufunguzi na pia wakatenga muda wao tena kutembelea maonesho haya.

Ndugu Wananchi,

Wakati wa uzinduzi wa maadhimisho haya, tulieleza kwa upana na kwa kutumia takwimu mafanikio ambayo tumeyapata katika Nyanja za uchumi, kijamii na kisiasa. Ni matumaini yangu kwamba maonesho yamesaidia kuthibitisha yale tuliyoyasema. Naomba kutumia fursa ya kufunga maonesho haya kuwaeleza kwa ufupi Watanzania mafanikio ambayo Tawala za Mikoa na Serikali za Mitaa imeyapata.

Ndugu Wananchi,

Tangu tupate Uhuru miaka 50 iliyopita, sekta ya Tawala za Mikoa na Serikali za Mitaa imepata mafanikio katika nyanja mbalimbali. Mojawapo

ya mafanikio haya ni kuanzishwa kwa Mpango wa Uboreshaji wa Mfumo wa Serikali za Mitaa ulioanza mwaka 1998 ambao ulilenga katika Kupeleka Madaraka kwa Wananchi. Dhana ya Upelekaji wa Madaraka kwa Wananchi imeelezwa kwa kina zaidi katika Sera ya Uboreshaji wa Mfumo wa Serikali za Mitaa ya mwaka 1998. Katika Sera hii, Mamlaka za Serikali za Mitaa, zinapewa uhuru wa kufanya maamuzi mbalimbali yahusuyo utoaji wa huduma kwa wananchi walio katika Mamlaka zao na kuwashirikisha katika kujiletea maendeleo na ustawi wao kwa ujumla. Pamoja na kupewa uhuru huo, Mamlaka za Serikali za Mitaa zinatakiwa kuutumia uhuru kwa kuzingatia Katiba na Sheria za nchi na endapo zitakwenda kinyume chake, Serikali Kuu inao wajibu wa kikatiba na kisheria kuingilia kati na kuchukua hatua dhidi ya Mamlaka hizo.

Ndugu Wananchi,

Mpango huu umeonyesha mafanikio katika nyanja za usimamizi wa fedha, rasilimali watu, ushiriki wa wananchi katika shughuli za kisiasa pamoja na mahusiano kati ya Serikali Kuu na Serikali za Mitaa.

Kufuatia kuimarika kwa dhana ya ushirikishwaji wananchi katika utawala wa nchi, kupitia mamlaka za Serikali za Mitaa na azma thabiti ya Serikali ya kuzijengea uwezo Mamlaka hizo. Serikali imekuwa ikiongeza mgao wa fedha za bajeti kwenda katika Mamlaka za Serikali za Mitaa. Mwaka 2004/05 wakati mfumo wa kutoa ruzuku unaanza jumla ya sh. Bilioni 4.8 zilitolewa kwenda katika mamlaka hizo. Kiwango hicho kimeongezeka mwaka hadi mwaka. Mwaka 2011/12 Serikali itapeleka takribani shilingi tirioni 3 sawa na asilimia 25 ya bajeti ya Serikali. Mafanikio haya ni makubwa na hivyo kuifanya Tanzania kuwa ni nchi ya kwanza katika nchi za Pembe ya Afrika katika kupeleka rasilimali fedha kwenye Mamlaka za Serikali za Mitaa.

Aidha, uwezo wa kusimamia rasilimali za umma katika mamlaka hizo pia umeongezeka. Kutokana na kuimarika kwa uwezo huo, Mamlaka za Serikali za Mitaa zinazopata hati chafu, zimeendelea kupungua kutoka 20 mwaka 2004/05 hadi 1 mwaka 2008/09. Mwaka 2010/11 Mamlaka nne za Serikali za Mitaa ndizo zilizopata hati chafu.

Ndugu Wananchi,

Hii haina maana kwamba tumeridhika sana na mafanikio hayo. Bado tunahitaji kujidhatiti ili kuwezesha Mamlaka hizo kuwajibika zaidi na hivyo kuongeza kasi ya kuwaletea wananchi maendeleo.

Ndugu Wananchi,

Hamasa ya wananchi kushiriki katika mchakato wa demokrasia katika mamlaka za Serikali za Mitaa ni kubwa. Mafanikio makubwa yamepatikana katika chaguzi za Serikali za Mitaa mwaka 2004 na mwaka 2009. Mwaka 2009 jumla ya vyama 17 vilivyosajiliwa vilishiriki kugombea nafasi 294,499. Nitoe wito kwa wananchi kuendelea kushiriki katika chaguzi zinazofuata. Aidha, baada ya chaguzi hizo kufanyika, tushiriki katika vyombo vya kisheria kusimamia utendaji wa Mamlaka za Serikali za Mitaa. Jukumu na wajibu wa kusimamia mamlaka za Serikali za Mitaa ni letu sote na wala si la viongozi wanaochaguliwa pekee.

Ndugu Wananchi,

Ili kuboresha uwajibikaji ndani ya Mamlaka za Serikali za Mitaa, Serikali inaandaa mabadiliko ya Sheria na Kanuni za Uendeshaji wa Mamlaka hizo ili kuwezesha Waheshimiwa Madiwani, ambao ni Wenyeviti wa Kamati za Maendeleo za Kata kuwa wanatoa taarifa za maendeleo za Kata zao ndani ya Baraza. Nimatumaini yetu kwamba hii itasaidia kuwafanya

Waheshimiwa Madiwani kuwajibika zaidi katika kuzisimamia Halmashauri za Vijiji/Mitaa katika Kata zao. Aidha, sambamba na utaratibu huo Waheshimiwa Madiwani watapewa fursa ya kuuliza maswali ya papo kwa papo kwa watendaji katika Mamlaka zao.

Ndugu Wananchi,

Ni wazi kwamba Mamlaka za Serikali za Mitaa ziliweza kutekeleza kwa mafanikio makubwa azma ya kujenga shule za sekondari za kata na kufanikisha azma hiyo vizuri. Hivyo basi, Serikali Kuu na wananchi kwa ujumla hatuna budi kuendeleza mafanikio hayo kwa kushirikiana na Mamlaka hizo katika kuimarisha na kuzipatia Miundombinu inayohitajika shule hizo.

Ndugu Wananchi,

Pamoja na mafanikio hayo zipo changamoto kadhaa hasa katika usimamizi wa fedha na kufanyika kwa vikao vya kisheria katika Mamlaka hizo. Serikali inatoa wito kwa Viongozi na Watendaji katika Mamlaka za Serikali za Mitaa, kuhakikisha kwamba vikao vya kisheria vinafanyika ili kutoa fursa kwa wananchi kushiriki katika kufanya maamuzi juu ya mambo yanayowahusu. Aidha, nitoe wito pia kwa wananchi kuitika wito wa kushiriki katika vikao pale tunapopewa wito wa kufanyika kwa vikao husika.

Ndugu Wananchi,

Serikali itaendelea kuwachukulia hatua wasimamizi wa Mamlaka za Serikali za Mitaa ambao watabainika kukiuka Sheria, kanuni na taratibu za usimamizi wa fedha na mali za Mamlaka hizo. Wananchi pia mnayo fursa kisheria ya kuhoji kuhusu mapato na matumizi ya fedha katika Mamlaka za Serikali za Mitaa kupitia Mikutano Mikuu ya Kijiji au Mtaa na

pia kupitia uwakilishi wa Waheshimiwa Madiwani katika Vikao vya Mabaraza ya Madiwani.

Ndugu Wananchi,

Katika kutambua nafasi ya Serikali za Mitaa katika kuleta maendeleo ya wananchi, mwaka 2005 Serikali iliamua kwamba kila ifikapo tarehe 1 Julai ya kila mwaka iwe ni kilele cha Siku ya Serikali za Mitaa nchini pote. Katika kipindi hiki, Serikali za Mitaa hupata muda wa kujitathmini pamoja na kueleza mafanikio yaliyoyapatikana kwa Wananchi wake. Sherehe hizi hufanyika katika Halmashauri zote na kitaifa hufanyika katika Halmashauri ambayo huchaguliwa wakati wa Mkutano Mkuu wa Jumuiya ya Tawala za Mitaa Tanzania (ALAT). Serikali itaendelea kuhakikisha kwamba Halmashauri zote zinafanya maadhimisho ya Siku hii ili kutoa fursa kwa wananchi kufahamu Halmashauri zao zinavyotekeleza majukumu yao pamoja na changamoto zinazozikabili.

Ndugu Wananchi,

Ili kusogeza huduma za kijamii na kiutawala karibu zaidi na Wananchi, Serikali imekuwa ikiongeza maeneo mapya ya utawala kadri inavyoonekana kwamba inafaa na kwa kuzingatia vigezo vilivyowekwa. Wakati Tanganyika inapata uhuru wake ilikuwa na majimbo tisa ya Utawala ambayo yalirithiwa toka utawala wa kikoloni wa Kiingereza. Mwaka 1966, Rais wa Awamu ya kwanza Hayati Mwalimu Julius K. Nyerere kwa Mamlaka aliyopewa, aliunda Mikoa 17 na kuondokana na utaratibu wa mgawanyo wa nchi katika Majimbo. Hadi sasa Tanzania Bara ina Mikoa 21, Wilaya 114 za utawala na Mamlaka za Serikali za Mitaa 133. Kutokana na kusudio la kuanzishwa kwa Mikoa mipya minne ya Katavi, Njombe, Geita na Simiyu na Wilaya mpya 19 Tanzania Bara itakuwa na jumla ya Mikoa 25 na Wilaya 133 baada ya mchakato mzima

wa kuanzishwa kwa maeneo haya kukamilika. Aidha, baada ya mchakato huu Mamlaka za Serikali za Mitaa zitaongeka hadi kufikia 166. Tayari Mheshimiwa Rais wa Jamhuri ya Muungano

wa Tanzania ametoa kusudio la kuanzishwa kwa maeneo haya chini ya kifungu cha 4 cha Sheria ya Maeneo mapya ya Utawala, Sura 397 ya Toleo la 2002 kwa Tangazo la Serikali Na. 285 la tarehe 9 Septemba 2011 kwa ajili ya uanzishaji wa Mikoa na vilevile, Tangazo la Serikali Na. 287 la tarehe 9 Septemba 2011 kwa ajili ya uanzishaji wa Wilaya. Madhumuni ya Notisi hizi ni kuzialika Taasisi, makundi ya watu au mwananchi yeyote ambaye ataguswa na uanzishaji huo kutoa maoni katika kipindi cha siku 21 kwa mikoa mipya na siku 30 kwa Wilaya mpya kuanzia tarehe ya Tangazo hilo. Nawashukuru wananchi wote walioshiriki katika kutoa maoni yao kwa maandishi na kuyawasilisha Ofisi ya Waziri Mkuu, Tawala za Mikoa na Serikali za Mitaa.

Ndugu Wananchi,

Mwaka 2009, Serikali iligatua usimamizi na uendeshaji wa elimu ya Sekondari kwenda katika Mamlaka za Serikali za Mitaa. Uamuzi huu unatokana na ukweli kwamba hivi sasa karibu kila kata ina shule ya sekondari. Hali hii inatokana na ushiriki wa wananchi katika ujenzi wa shule hizi. Hata hivyo wapo watu wenye mitazamo hasi ambao wanabeza uwepo wa shule hizi. Sote tumeshuhudia kuwepo kwa wanafunzi waliofanya vizuri katika mtihani wa kidato cha sita mwaka 2011 ambapo kati ya wanafunzi 20 waliofanya vizuri wanafunzi 7 wanatoka katika shule za sekondari za kata. Changamoto zilizopo katika Shule hizi zitatumika kupata ufumbuzi wa matatizo yaliyopo. Masuala ya sera, viwango, mipango na tathmini na ufuatiliaji yataendelea kusimamiwa na Wizara ya Elimu na Mafunzo ya Ufundi.

Ndugu Wananchi,

Mwisho, napenda kuwashukuru sana wale wote ambao wametuunga mkono katika kipindi hiki cha miaka 50 iliyopita na kutufikisha hapa tulipo. Tuendelee kulinda mafanikio tuliyoyapata na kuzitumia changamoto tulizokabiliana nazo kama chachu ya kusonga mbele. Asanteni sana kwa kunisikiliza na natangaza rasmi kwamba maonesho haya yamefungwa.

TUMETHUBUTU, TUMEWEZA NA TUNAZIDI KUSONGA MBELE.